

HABARI ZA MITI NA MITISHAMBA MIONGONI MWA WAMIJIKENDA NA WASWAHILI—MATOKEO YA KWANZA KUTOKA UTAFITI

ULRICH SCHULZ-BURGDORF

Utafiti ambao ni msingi wa habari hizo umefanywa katika miezi za Oktoba mpaka Disemba 2000 katika wilaya wa Kwale na Kilifi huko nchi ya Kenya. Wanachama wa timu ya utafiti wetu walikuwa Prof. F. Rottland, ambaye aliweka taratibu msamiati wa miti uliokusanywa, na Bw. Mohamed Pakia ambaye ni mwanabiolojia na aliyehojiana wanafunzi wa shule ya sekondari kuhusu ujuzi wa miti na mitishamba wao. Bw. Pakia ameshafanya kazi katika Coastal Forest Conservation Unit, yaani watu ambao husaidia wazee wa kimijikenda katika kuhifadhi misitu mitakatifu inayoitwa “makaya” na inatumiwa kwa matambiko na kama makaburi. Misitu ya makaya ni maeneo yenye miti mingi ya aina mbalimbali na wanyama maalum ambao huishi hapo hapo tu. Ni maeneo yenye “biodiversity” na ni mabaki ya “Sansibar-Inhambane Forest” ambayo zamani imeenea kutoka nchi ya Somalia mpaka Msumbiji.

Siku hizi ziko hatari kwa misitu ya makaya kama (kwa mfano) kujenga nyumba na hoteli ya kitalii katika maeneo ya Kaya Chale ambapo ni katika kisiwani cha Chale na nusu ya kisiwa imeshauzwa na mwenye hoteli wa kizungu. Hatari nyingine katika wilaya ya Kwale ni mpango wa kujenga kiwanda cha titanium metal bila kupima athiri kwa mazingira ya miti, maji, ardhi, wanyama na wanadamu. Juu ya hayo iko hatari ya tofauti ambayo Bw. Pakia ametambua: Ni hatari ya kupoteza ujuzi wa miti na mitishamba iliyotumiwa namna ya kimila miongoni mwa wanafunzi wa shule ya sekondari: vijana hawajui matumizi ya mimea na pia wamepotea moyo wa kutaka kujua mambo hayo.

Mimi mwenyewe nimefanya utafiti miongoni mwa watuwazima na wazee katika wilaya wa Kilifi. Nimeuliza wapaji habari kumi na nane katika umri wa ishirini na tisa mpaka sitini au juu kutoka makabila mbalimbali kama Wachonyi, Wadigo, Wajibana, Wakauma kwa mfano. Miongoni mwa wenye umri huu nimetambua kwamba hakuna kupoteza au msiba wa ujuzi wa kutumia miti na mitishamba na njia ya kuikuza au kutunza. Katika habari zifuatazo ninatoa mifano ya ule ujuzi wa watuwazima na wazee. Siyo rahisi kujibu swali kwa nini wanafunzi hawajui au wasema wasijue mambo ya matumizi ya miti na mitishamba. Hakuna shida wazazi wao hujua mambo hayo. Labda baada ya kurudi vijijini na wamekua kuwa watuwazima wanafunzi wanapewa ujuzi wa ukulima na uganga. Ni tofauti baina ya ujuzi wa shule na ujuzi yaani ujuzi wa kibiolojia na ujuzi wa maarifa wa kienyeji ambao pia huitwa “folk knowledge” au “folkbiology” unaonezwa bila kwenda shule. Sasa, inaonekana kwamba ni wanafunzi wa shule tu ambao wamefunzwa kwamba miti yenye majani tu, yaani “chlorophyll” au “green matter” ina uwezo wa kubadilisha “carbondioxide” iwe “oxygen” na huweza kutengeneza

matter” ina uwezo wa kubadilisha “carbondioxide” iwe “oxygen” na huweza kutengeneza chakula chao kwa msaada wa mwangaza au nuru ya jua. Habari hizo zilinipewa na mpaji habari mmoja ambaye ni tabibu au mganga mswahili na ambaye alifanya kazi ya mwalimu wa shule ya sekondari kabla ya kuanza kufanya kazi ya utabibu. Yeye pia alinisaidia katika kutafsiri na kufahamu habari zilizopewa na Wamijikenda. Kwa walio wengi wa wapaji habari wa kike na wa kiume kazi ya kutengeneza chakula ambacho miti lazima kuwa nacho, ni kazi ya mizizi, siyo kazi katika majani. Lakini wapaji wa habari hizo pia walifikiri kwamba nuru ya jua na upepo pia ni muhimu kwa miti ikue. Kwa kupata chakula na maji mizizi ya miti lazima “kutembea” katika ardhini. Kwa wao waliofikiri hivyo, mizizi ni sehemu ya uhai na roho katika miti. Kazi ya mizizi pia imeelezwa kama “kushika”, “kuchukua”, “kunyonya” au “kuvuta” chakula. Wengine walisema kwamba kazi hii ni kama “kupenya ardhi” na “kupandisha chakula juu”. Mpaji habari mwingine, aliyemaliza shule ya sekondari, alitumia dhana ya “capilarity” kwa kueleza uwezo wa kutoa maji na madini kutoka mchangani na kuyapeleka sehemu za juu. Na mwingine alilinganisha kazi ya mizizi na mambo ya binadamu akasema kwamba kazi hii ni kama “kutia chakula mdomoni” na “kukitafuna na kukimeza chakula”.

Sasa, ni jambo la kuvutia kwamba hakuna tofauti baina ya wanafunzi wa shule ya sekondari na watuwazima kuhusu mimea huitwa “magugu” na “uyoga”, yaani “weeds” and “mushrooms”. Inaonekana kwamba hakuna majina maalum kwa mimea hiyo chini ya kiwango cha magugu na uyoga. Aina mbalimbali za uyoga huitwa “uyoga” tu. Neno la “magugu” limeelezwa kama “manyasi ambayo huliwa na wanyama au ng’ombe”. Kwa Mchonyi mmoja magugu kwa mfano ni kama mti ambao huitwa “chadza”, yaani mti ambao “haiwezi kufanyia kazi yo yote”. Kwa mtu mwingine magugu ni “mimea ambayo haitakikani mahali ilipomea” na lazima kuipalia. “Uyoga”, yaani mushrooms, kwa walio wengi huwa ni “vyakula vya porini” ambayo pamoja na mimea mingine “inamea kwa Mungu”. Baadhi ya uyoga huliwa na zina ladha tamu sana, nyingine za sumu haiwezekani kuzikula. Pia mimea hiyo imeelezwa kuwa “miti isiyo mwenye matawi” na “isiyoweza kuhimili jua kali” au yenye “sura kama mwavuli” na ambayo “hukua kandokando ya ziwa na mahali pengine palipooza”.

Ni wazi kwamba iko tofauti baina ya elimu na madhana ya shule ya sekondari na ujuzi wa kimila au kawaida ambayo hutumiwa katika kueleza mambo ya kimaumbile. Wanafunzi wanatumia msamiati ya kisayansi kama “chlorophyll”, “carbondioxide”, “oxygen”, “capilarity” kwa mfano. Madhana hayo waenyeji ambao hawakuhudhuria masomo ya shule hawajui. Lakini katika maisha ya kawaida mara nyingi siyo lazima kuweza kueleza mambo kwa njia ya kisayansi ikiwa watu wanatumia ujuzi wao katika ukulima. Inawezekana maelezo ya kimila siyo kweli kutoka msimamo wa sayansi au ujuzi wa shule. Lakini ujuzi wa kienyeji au kimila una uhusiano na mazoezi na vitendo vya ukulima na maarifa kutoka kulima. Na katika mambo hayo waenyeji ambao hufuata maarifa yao, wanafaulu kila mara wakitumia binu zao kwa mfano za kukuza miti maalum pamoja, za kupalilia, za kutumia mbolea za kimaumbile na hatimaye wapate mavuno mazuri. Juu ya hayo, sehemu za ujuzi wa shule zinaenezwa ziingie katika ujuzi wa kawaida kwa njia ya mazungumzo. Na shauri kutokana na

ya mchanganyiko wa ujuzi wa shule na ujuzi wa kimila au kawaida. Katika jambo hilo ni kama mwanafalsafa ya kisayansi jina lake ni Ludwik Fleck alivyosema: watu wote ni wanachama wa "cognitive collective", yaani kundi la kufikiri na kuzingatia mambo ya ulimwengu na maisha ya binadamu na ambao huwasiliana fikra zao kila siku. Na utaratibu huo pia unatokea baina ya wapaji habari wa kienyeji na mwenye utafiti kutoka nje.

Marejeo:

Medin, Douglas L. & Scott Atran. 1999. *Folkbiology*. Cambridge, Ma: MIT Press.

Fleck, Ludwik. 1980. *Entstehung und Entwicklung einer wissenschaftlichen Tatsache. Einführung in die Lehre von Denkstil und Denkkollektiv*. Frankfurt: Suhrkamp.

